



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU UTEUZI WA MADIWANI WANAWAKE WA VITI MAALUMU


Zanzibar, 20 Aprili, 2026

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 57(1) na 113 vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake kilichofanyika tarehe 20 Aprili, 2026 imefanya uteuzi wa madiwani wanawake wa viti maalumu watano (05) kama ifuatavyo: -

- i. Ndugu **Gema Gervas Ishengoma** wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Diwani wa Viti Maalumu katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;
- ii. Ndugu **Janeth Shadrack Sinyangwe** wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Diwani wa Viti Maalumu katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga;
- iii. Ndugu **Zainabu Martin Siame** wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kuwa Diwani wa Viti Maalumu katika Halmshauri ya Mji Tunduma;
- iv. Ndugu **Paulina Stephano Nalingigwa** wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Diwani wa Viti Maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai; na
- v. Ndugu **Sikudhani Japhari Kolongo** wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Diwani wa Viti Maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

Tunawatakia kila la heri madiwani wote wateule.

Imetolewa na:


Kallima, R. K.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

